# Ilahhaslidu gu Burungaisoo

## (Methali za Kiburunge)



Lugha: Kiburunge

Gimba gu Burungaisoo

Cocoanee Burungaisoo

**Kichwa**: Ilahhaslidu gu Burungaisoo
Methali za Kiburunge / Burunge Provebs
**Lugha:** Kiburunge
**Waandaaji:** Timu ya Waburunge 2011
**Michoro imetoka**: "The Art of Reading" 2.0
© SIL International, 2001 Imetumiwa kwa ruhusa
**Toleo la** kwanza / First edition
**Nakala** 100
© SIL International, 2011
S.L.P. 1369, Dodoma, Tanzania.

# Ilahhaslidu gu Burungaisoo
# (Methali za Kiburunge)

Huduma ya Kuendeleza Lugha za Makabila,
Mkoa wa Dodoma
S.L.P. 1369, Dodoma, Tanzania.
East Africa.

# Utangulizi

## (Gimba guri giyaada)

Kitabu hiki kimeandaliwa mahususi kwa ajili ya Waburunge wanaopenda kujifunza jinsi ya kusoma na kuandika lugha yao. Mtu yeyote, ambaye amejifunza jinsi ya kusoma na kuandika lugha ya Kiburunge, anaweza kukitumia kitabu hiki.

# Shukrani

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa waandaaji wa kitabu hiki cha methali za Kiburunge, ilahhaslidu gu Burungaisoo.

Vitabu vyote vinapatikana katika ofisi zetu, Goima karibu na kituo cha basi, Kondoa Choka gesti na Dodoma karibu na MAF.

**1. Amasi na ilii mogombaiimaa.**

Usiku ndipo penye utasa.

**Maana:** Mtu apatwapo na shida usiku, si rahisi kupata msaada wa haraka, lakini mchana ni rahisi kwa sababu watu ni wengi.

**2. Amasi sigoó baloo de'enaaba.**

Mambo ya usiku hayajulikani.

**Maana**: Mtu anapolala usiku, hajui kinachotokea au kesho kukicha kutatokea nini.


**3. Aalimiiso'oo da sira hiitlaakhwi.**

mwanamke mrithi ana makalio mapana.

**Maana:** Mwanamke mrithi, huwanyanyasa watoto yatima, na humiliki kwa nguvu.



**4. Bawdiisee noó ya'ay kosi omina.**



Mtu mjinga ndiye aleaye watoto wake.

**Maana:** Mtu asiye penda ugomvi, dhuluma, lawama, ukorofi wa aina yoyote na watu. Huishi maisha marefu, na hata hutuliza akili kuwalea watoto wake.

**5. Baloo gari sla'ay wante, hangini ilii gusitay haa kumbo'oo.**

Siku ambayo upo uchi, ndiyo siku ambayo unakutana na mkwe.

**Maana:** Siku ambayo hauna kitu nyumbani, ndipo wageni hukujia, au ndipo shida hukujia.

**6. Cuuru gu danaa'googu haguri hhanti hha�aluta.**

Usiringie kiota cha mwenziyo.


**Maana:** Usiringie kitu chochote cha kuazima, maana mwenyewe anaweza kukichukua wakati wowote. Jivunie chako japo si kizuri.

**7. Cufa da heedi da kaari.**

Jasho la mtu ni la thamani.

**Maana:** Kazi yoyote anayoifanya mtu ni ya thamani huwa haipaswi kudharauliwa kwa njia yeyote ile.

**8. Dahaa waoo sigi hhanti tla'amuta.**




Wageni ni wapitaji tu usiwaogope.

**Maana:** Wageni ni baraka, na ni wa kupita tu. Wanapokuja nyumbani hula chakula na kukiacha usiwaogope.

**9. Dagara na kere'ediye.**

Mguu ndio ukatike.

**Maana:** Kumsisitiza mtu au watu kukimbia kwa nguvu inapotokea hatari ili wajiokoe au pia wakaokowe kitu fulani.



**10. Daw yoó /aginaaba qafiru leẽ.**

Tembo huwa hali ganda moja.

**Maana:** Mtu akiwa na shida hachagui aina ya msaada. Huchukua chochote ilimradi tu kimsaidie.

**11. Diidaw yaa ki/i sa sluufaa.**

Simba alirudi kwa ajili ya kula majani.

**Maana:** Tajiri anapokuwa maskini, hukumbuka makombo aliyokuwa akitupa wakati wa utajiri wake.

**12. Dihhay bee, maraai maraai.**


Mtu aitwaye Mkali alisema kwamba, nyumba na nyumba.

**Maana:** Kila mtu ana tabia yake hakuna mtu anayefanana kitabia na mtu mwingine.

**13. Dinca yoó gaasida.**

Kidole kinaua.

**Maana:** Mtu mwovu, mkorofi, anayependa kufanya fujo huuawa haraka sana na watu.



**14. Digimaa sugoó gaasi.**

Mpaka husababisha kifo.

**Maana:** Watu wanapogombea mpaka wa shamba au kiwanja, husababisha ugomvi, na hata kifo wasipopatana.

**15. Dooslimiisay haroó kooloo gosi ilagwaai.**

Mkulima hufa na jembe lake.

**Maana:** Mtu mwenye bidii hujilisha yeye mwenyewe.



**16. Eea kontaaba kitiĩ, baku eea sagaa qaasiiba kitiĩ.**

Sikio halina kiti au sikio halikuwekewa kiti.

**Maana:** Sikio halina mipaka katika kusikia, husikia lolote lisemwalo, hata lile linalosemwa mahali pa siri.

**17. Eea na taatli.**

Tega sikio.

**Maana:** Kumsisitiza mtu asikilize kwa makini yanayo zungumzwa, au yanayo tetwa juu yake, au juu ya mtu mwingine.



**18. Fitlaaloota dagaroó ibiidiyaaba khoorooge.**

Ukorofi hautakiwi duniani.

**Maana:** Si vema kuishi na tabia mbaya na wenzako hapa duniani.

**19. Fitlaalootusay yoó saga daasiyaaba.**

Mharibifu huwa haishi maisha marefu.

**Maana:** Mtu mharibifu asiye na maisha mazuri na wenzake, yaani ni mkorofi, mwizi, mjeuri, mgomvi, mchonganishi mpiganaji huwa hana maisha marefu.

**20.Gimba du/iya .**

Maneno ni mafuta.

**Maana:** Maneno mazuri hufariji, hujenga, hutia moyo, ni kama vile mafuta, ambayo hufanya ngozi ya mwili kuwa nyororo.



**21. Gimba kologoo gooba tuba, yoó ilasliqi rawaa gu khaimooge.**

Maneno siyo kipande cha mti kwamba, kinaweza kukwama juu ya mti.

**Maana:** Maneno yakiisha kusemwa, hayakwami au hayapotei hewani yatafika tu kwa mtendewa.

**22. Gura'a cokhoriisay.**

Tumbo ni chonganishi.

**Maana:** Kwa sababu ya njaa au tamaa ya tumbo, tumbo husababisha mtu kuiba, hatimaye husababisha kumpeleka mtu mahali pa baya na hata kufungwa.

**23. Gura'a fitlalootuusee.**


Tumbo ni haribifu.

**Maana:** Kazi ya tumbo ni kupokea vyakula vya aina mbalimbali, lakini tumbo haliweki akiba.

**24. Gura'a hindaqaru.**

Tumbo ni tajiri.

**Maana:** Tumboni huingia vyakula vingi mno vya kila namna.



**25. Gura'a kwa'alimoo, yoó unaaba.**

Tumbo ni masikini huwa haliridhiki.

**Maana:** Tumbo hushibishwa sana, lakini baada ya muda mfupi, huhitaji tena kula.

**26. Hadee konkiya yoóti khodikhodita dagaroó maciyaaba.**

Mwanamke ni kama kuku anatafuta tafuta kila mahali hawezi kushindwa.



**Maana:** Mwanamke ni Kama vile kuku anavyo watunza vifaranga vyake. Mwanamke mjane hutunza watoto wake vema kuliko mwanamme mjane.



**27. Heedi gu gura'a /abaaku.**

Mtu mwenye tumbo jeupe.

**Maana:** Mtu mkarimu, mwenye roho nzuri, mpenda watu, msamaria na mwenye kuwasaidia watu.

**28. Heedi gu gura'a hii boo/u.**

Mtu mwenye tumbo jeusi.

**Maana:** Ni mtu mchoyo, mwenye roho mbaya, mchawi, asiyependa watu, mweye chuki.

**29. Hotu hadee mungiya da anda.**

Mtoto wa kike ni mumunya tamu.

**Maana:** Mtoto wa kike ana roho ya huruma sana.

**30. Hotu hadee pa/adiya.**

Mtoto wa kike ni mbegu inayoruka.

**Maana.** Msichana anapo olewa huenda mbali sana kuanza maisha mapya sehemu nyingine.

**31. Hhadaa da Iliitleemu dagoó taatliyaaba.**

Fimbo ya Mungu haikingwi.

**Maana:** Mungu ana uwezo wa kufanya jambo lolote, tena Mungu anapoamua kutenda au kafanya jamba lolote, hakuna awezaye kulizuia.

**32. Hidaqaruumaa rau.**

Utajiri ni umande.

**Maana:** Utajiri ni kama vile umande ambao hutanda juu ya majani asubuhi. Lakini mara jua likiwaka umande wote hutoweka. Mtu anaweza kuwa tajiri leo lakini kesho akawa maskini

**33. Hhanti hha'aluta hari hhaysoo.**

Usiringie mkia.

**Maana**: Usiringie utajiri ulionao, au cheo ulicho nacho si vema, maana siku ukifa utajiri huo utauacha.

**34. Ilamuree sagaa gaasi kuumba'a dokonge.**

Aibu ilimsababisha mkwe kuuawa kwenye shimo la takataka.

**Maana:** Usione aibu au haya kuomba msaada kwa mwenzako unapo kuwa na shida, njaa, tatizo au hitaji lolote. Ukiona haya mwisho utaiba, na kujiingiza hatiani.

**35. Ila na kihhe.**

Uma jicho.

**Maana**: Kumsisitiza mtu, atazame kwa makini, uangalifu kitu kinacho tendeka, kinachofanywa na watu au mtu.

**36. Ilaa konaaiiba pingimoo.**

Macho hayana mfuniko/pazia.

**Maana:** Macho huona kila mahali, hayana mipaka katika kuangalia.

**37. Karahhasi muuna, muuna na khupisi.**

Shika sana moyo, funika moyo.

**Maana:** Jipe moyo usiogope, ondoa wasiwasi, mashaka na hofu.

**38. Kiiki/imisu sugwaa slay sagadahhama.**

Kurudirudi mahali kunaweza kukusababisha kupata matatizo.

**Maana:** Ukishaaga mahali ukaondoka usirudi, unaweza kukutana na tatizo lingine au jambo baya likakuingiza hatiani.

**39. Koisa naa daw gaasidi.**

Kujaribu kuliweza kumwua tembo.

**Maana:** Usiogope kufanya jambo, hata kama ni kubwa au ni gumu, jaribu tu, na mwisho unaweza kupata mafanikio.

**40. Kofiyaa hagari hhanti dumbuta, hagari hhanti hha'aluta.**

Usijivunie kofia uliyo nayo.

**Maana:** Ukiwa na cheo au madaraka ya aina yoyote, usiringe nayo, na kuwadharau wengine kuwa si kitu. Wakati wowote waweza kushuka au kushushwa toka madarakani na kuacha cheo chako.



**41. Kooloo yoóy facakusi kwaahhago.**

Jembe huteleza toka begani.

**Maana:** Mtu ambaye alikuwa ni tajiri kifedha, mifugo, mazao. Vikiisha, hujikuta ameingia katika shida, taabu na mahangaiko mengi ambayo hajawahi kukutana nayo.

**42. Kona urunga.**

Ana pua.

**Maana.** Ni mtu mwenye kiburi, mkorofi na mwenye sifa mbaya.

**43. Konto/iya yaa gointi mara.**

Udongo umezuia nyumba.

**Maana:** Udongo, yaani ukuta wa nyumba unazuiya mambo mazuri na mabaya yasionekane. Si rahisi mtu kujua maisha ya watu wengine ndani ya nyumba yao, mpaka ameishi nao kwa karibu zaidi.



**44. Khooroo sira da dahhaã yoóti niini/imita.**

Dunia kitako cha kipeyu huwa inazunguka.

**Maana:** Maisha ya mwanadamu ni kama vile kipeyu kikiwekwa kinazunguka.

**45. Khoroo unjuwaaliya.**

Dunia kicheche.

**Maana:** Usimcheke mwenzako anapo patwa na shida au matatizo, nawe pia yanaweza kukupata wakati wowote. Leo kwangu kesho kwako.

**46. Kwa'aluumaa Cuma.**

Umaskini ni kama uchafu.

**Maana:** Usimdharau mtu maskini anaweza kuwa tajiri wakati wowote.



**47. Lakalakaa sagaa slaslakhi mokotiya.**

Haraka haraka ina sababisha kuangusha mzigo.

**Maana:** Usifanye uamuzi au usitende  jambo kwa haraka bila kufikiri.

**48. Lawaalimoo yoó kweera de'ena.**


Mchungaji huchunga pori.

**Maana:** Mtu aendapo kuchunga, hukutana na hatari mbalimbali.

**49. Letuti duguũ ilii pisi.**

Leo umepambazukiwa.

**Maana**: Mtu aliyezoea kufanya mambo mabaya kwa siri, ipo siku atabainika wazi. Au Mtu kabahatika kupata kitu bila kutegemea.



**50. Losona dugoó losonuusiyaaba mara lenge.**

Sherehe huwa haifanywi katika nyumba moja tu.

**Maana:** Shida, matatizo au kifo, huwa si ya mtu mmoja.

**51. May hida /agineei dabaiĩ koku.**

Waache watu wale mikono yako.

**Maana:** Kuwa mkarimu kwa kuwasaidia watu, katika shida zao mbalimbali.

**52. May hiiwanquda loo/iya.**


Usivuke jani.

**Maana:** unapoonywa sikia, sikiliza maonyo usiyapuuze.

**53. Mahhatu gu amoo gu hhanti iliikubahhada.**

Kivuli cha njiani usikinyee.

**Maana**: Usimdharau jirani yako hata kama ni maskini lakini anaweza kukufaa siku moja.



**54. Mokonkonimoo yoóy napa/i diĩ bi/inaage.**

kunguni hujificha kimiya kibambazani au ukutani.

**Maana:** Usilopoke maneno ovyo, kusengenya watu, kwa kusema maneno mabaya juu ya mtu mwingine, kumbe kuna mtu anakusikiliza, bila wewe kujua.

**55. Muuna yoó dakusi mara gosi.**

Moyo hukosa nyumba yake.

**Maana:** Usifanye jambo kwa hasira, fikiria kwanza, maana hasira ni hasara.

**56. Muuna gwaslara.**

Moyo ni mganga, mtabiri.

**Maana:** Moyo unapo sita kwenda mahali, au kufanya jambo fulani, usiulazimishe.

**57. Nanku hhawata mungumoo gu qada.**


Mtoto wa kiume ni mumunya chungu.

**Maana:** Mwanaume hana huruma kama vile mwanamke

**58. Omeeri ningoó slaslayaaiiba.**

Milima haikutani.

**Maana:** Usimtendee mwenzako mambo mabaya, ukidhani hamtakutana tena, lakini ujue siku moja mtakutana, na utahitaji msaada wake.



**59. Pandaa dii boo/i aluũ gwii pisari.**

Mbele kuna giza nyuma kweupe.

**Maana.** Mambo yaliyopita unayafahamu, lakini mambo yajayo huyafahamu.

**60. Qaymoo da oday hingoó ina lenkosi ga/ayda.**

Shamba la udo hujilinda lenyewe.

**Maana:** Mtu mwenye tabia nzuri, hujilinda mwenyewe, hahitaji kulindwa.

**61. Suntima gu dana'a googu hagu hhanti qasayda.**

Mburuzo wa mwenzako usiucheke.

**Maana:** Usimcheke mwenzako anapopatwa na shida au tatizo.

**62. Slagaaduusay ha kweera nugoó /agida.**

Mwindaji huliwa na pori.

**Maana:** Mwindaji hufa katika mawindo, kama vile kuuliwa na wanyama wakali, au kung⍰atwa na nyoka.




**63. Slehheẽ gu gwehheeri /itima.**
Mwezi wa kuwanyima mbwa.
**Maana:** Huu ni mwezi ambao njaa huwa ni kali zaidi, watu hawasaidiani, hata mbwa kupewa tonge dogo ni shida.

**64. Slehheẽ gu /umaamu'u.**
Mwezi wa kununa.
**Maana: H**uu ni mwezi ambao chakula ndiyo kinaanza kuiva mashambani watu wanakula kisirisiri. Kiasi kwamba hata maganda ya mahindi, mamumunya, maboga hutumbukizwa kwenye mashimo marefu ili yasionekane na watu.

**65. Slehheẽ gu kekelaa.**
Mwezi wa vicheko.
**Maana:** Huu ni mwezi ambapo mazao mashambani tayari yameisha iva, na sasa watu wanakula hadharani bila tena kuficha wala kunyimana.





**66. Yaa tlo/osi gorogombimoo.**

Ameruka mtunduru.

**Maana:** Ameenda tohara, ameanza kuyaelewa maisha, ya kuwa mtu mzima, anajiongoza mwenyewe.

**67. Yaaee yoó leehhisida heedi hhoinayge, tlakwarooge.**

Mguu humpeleka mtu pabaya, pia humpeleka pazuri.

**Maana:** Mtu anapotembea huweza kukutana na mambo mema au mabaya.

**68. Ya/abimiisay konaaba saga dahhama.**

Mtu anayetumwa hana ngeu.

**Maana:** Atumwaye kupeleka maneno au ujumbe hana Lawama.

**69. /alu hiĩ fudui.**

Chungu kimefoka.

**Maana:** Pale alipopatengemea mambo yameharibika, hivyo hana tena msaada. Wamegombana.



**70. /atlimoo faraa gura'a kitanguru.**

Jino mfupa tumbo kibuyu.

**Maana:** Mtu huyaweka mawazo mazuri au mabaya moyoni mwake bila kusahau. Tena anaweza akawa anacheka na watu vizuri, lakini kumbe ana uchungu moyoni mwake.

**71. /agoo da hheehhisay dagoó hhanteege /agina.**
Chakula cha mtu mchoyo huliwa gizani.
**Maana:** Chakula cha mtu mchoyo hakiliwi na watu, kwa sababu huliwa gizani tena kwa kujificha.

**72. /agoo da cabuusay dagoó cenceege /agina.**
Chakula cha mtu mkarimu huliwa kwenye mwanga.
**Maana:** Chakula cha mtu mkarimu huliwa na watu wengi, na hakifichwi.



## Mengineyo

Tunakaribisha maoni, mapendekezo na ushauri kwa ajili ya kuboresha kitabu hiki na vingine vitakavyotolewa baadaye.

Tafadhali ukikuta kosa lolote ndani ya kitabu hiki, au ukiwa na swali au pendekezo lolote, au ukihitaji nakala nyingine ya kitabu hiki, wasiliana na:

Anna Saini, Goima karibu na kituo cha basi. Namba ya simu 0685-198409.

Au Ofisi ya Dodoma: SIL, S.L.P. 1369, Dodoma (karibu na shule ya msingi mlimwa A). Namba ya simu 0262350003. Na e-mail magdalena_damasi@sil.org.

Vitabu vingine vinapatikana katika ofisi zetu. Angalia nyuma ya kitabu hiki utaona orodha ya baadhi ya vitabu vya Kiburunge.

## Vitabu na kanda ambavyo vinapatikana katika huduma ya lugha ya Kiburunge.

- Sominee Burungaisoo
- Giyaadimiisay gu Burungaisoo
- Ruuti
- Yoona
- Iburayiimu
- Maariko
- Cheetatu gu Pawlo sa Timoteeyo Tiito haa Filemooni
- Ansaa da Goimaa
- Ansaa da Mirambu
- Ansaa da Pampay
- Ansaa da Cambalo
- Ansaa da Songolo
- Kanda
- Ruuti
- Yoona
- Raaˈamee da Iliitleemu



Shirika la SIL International limeenea katika maeneo mbalimbali, linahudumia lugha mbalimbali katika nchi zaidi ya 70 ulimwenguni kote. Zaidi ya mataifa 20 kati ya mataifa 70 yako Afrika.

Lengo la SIL ni kuinua utafiti wa kiisimu, maendeleo ya lugha, mafundisho ya kusoma na kuandika, utafsiri, pamoja na mambo ya kielimu na kutafiti utekelezaji wa huduma, kijamii na kimaendeleo. Kwa upande wa mkoa wa Dodoma tunatoa huduma kwa makabila ya Waburunge, Warangi, Wasandawe na Waalagwa.